# Kiswahili na Siasa: Uchanganuzi wa Ishara na Tamathali katika Tamthilia ya *Visiki* Kisemiotiki

*Sanja Leo Leonard*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza fasihi na siasa kupitia tamthilia ya Kiswahili. Lengo kuu la makala haya ni kuchanganua ishara na maana za kisiasa na jinsi zinavyojitokeza katika tamthilia ya *Visiki* kwa kutumia nadharia ya semiotiki, misimbo ya Barthes ya kiseme,kiishara na matukio. Kisemiotiki, ishara huathiri namna msomaji wa matini za kifasihi huishia kufasiri maana nasibishi ya kina ya matini. Tulifasiri ishara na uashiriaji katika tamthilia ya *Visiki* kwa sababu kisemiotiki, lugha ya kiishara huwa na uwezo wa kuwasilisha maana mbalimbali kwa njia ya uashiriaji. Kutokana na ufasiri huo wa ishara, makala haya yanajadili kuwa, wakati umefika ambapo siasa za bara hili zinastahili kubadilika na kuzingatia demokrasia za Kiafrika, haki za wapiga kura, za kibinadamu pamoja na kukumbatia maarifa mapya ya kisasa. Makala inahitimisha kwamba, Mataifa ya Kiafrika ni sharti yazinduke kisiasa na kukomesha lawama dhidi ya mataifa ya Kimagharibi kila yanaposhindwa kudhibiti hali nchini mwao.**

**Maneno Muhumu:** *Visiki*, *Mapisi, Siasa, Semiotiki,*

**Utangulizi**

Wamitila (2003) na Atkin (2013), wanashadidia ya kwamba, fasihi huashiria ukweli kwa njia ya kutumia ishara za lugha kwa njia ya ubunifu ili kumulika masuala muhimu ya kijamii. Wanachosema ni kwamba, fasihi huwa imefungamana na maisha ya kila siku ya wanajamii na huonyesha tajriba yao ya muda mrefu na hatua ambazo wamepiga kimaendeleo. Kulingana na *Kamusi ya Karne ya 21,* siasa huwa muhimu katika kutolea kauli za kisiasa na maamuzi muhimu yanayohusu utawala (*Ryan, A 2012, Van der Eijk, C 2018).* Tulifasiri ishara na uashiriaji katika tamthilia ya *Visiki* (Khaemba Ongeti) kwa sababu, lugha ya kiishara huwa na uwezo wa kuwasilisha maana mbalimbali nasibishi katika matini zinazochunguzwa (Bradford 1997). Aina hiyo ya lugha huathiri hisia za msomaji wa matini za kifasihi na namna anavyoishia kufasiri maana zinazowasilishwa (Wales 2011). Fasihi ni sanaa ya lugha (Mbuthia na Iribemwangi 2014). Kwa hivyo, lugha ya kiishara hutumiwa kufumba ujumbe na kuukoleza (Senkoro 1988). Ni kwa sababu hiyo ambapo tulifasiri ishara na tamathali za kisiasa katika tamthilia ya *Visiki* na Khaemba Ongeti (1984)

**Mapitio ya Maandishi**

Fasihi huwa na majukumu mengi kwa jamii (Wamitila 2003, Arege na Matei 2005). Mojawapo wa majukumu ya fasihi ni kutoa mwelekeo kwa jamii. Kupitia fasihi, wanajamii hueleza tajriba zao mbalimbali kuhusu maisha ikiwemo siasa na masuala mengineyo (Senkoro 1988). Fasihi kwa hivyo, ina dhima ya kufunza na kuielekeza jamii katika mwelekeo ufaao (Arege na Matei 2005). Kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana, ulimwengu wa fasihi ya Kiswahili katika kuzungumzia masuala kama: jamii na siasa umepanuka kitaifa pamoja na kimataifa (Iribemwangi na Mukhwana 2011). Fasihi huwa na uwezo wa kukiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuibua maana nasibishi ambazo huwa na maana za kina katika ufasiri wa ishara (Leech 1969). Mkutadha ambamo ishara inayofasiriwa huchipukia huwa na athari kwa ujumbe unaowasilishwa na namna ujumbe huo huishia kufasiriwa na mhakiki. Mabadiliko ya kiwakati huwa na uwezo wa kuathiri matini za kifasihi kidhamira, kimaudhui na kifani (Shariff 1988). Kiswahili hivi sasa kinatumika katika sehemu nyingi za ulimwengu kama lingua franka na kazi zake za kifasihi haziwezi kutengwa na matukio ya kilimwengu hasa siasa (Iribemwangi na Mukhwana 2011). Hiyo ndiyo sababu tulifasiri ishara na tamathali katika tamthilia ya *Visiki* kisemiotiki.

**Nadharia**

Barthes ndiye wa karibuni sana baada ya De Saussure, Peirce na Jakobson katika kutumia nadharia ya semiotiki kufasiri ishara. Kazi zake maarufu ni: *Writing Degree Zero* (1954) *Mythiologies* (1957), *The Death of the Author and Elements of Semiology* (1964) *The Fashion Systems* (1970), *The Pleasure of the Text* (1973), *S/Z* (1974) na *Lovers Discourse* (1977). Barthes alipendekeza kuweka matini za kifasihi katika vijisehemu vidogovidogo ambavyo aliviita leksia. Leksia hizo zilimwekea msingi wa kilichokuja kujulikana kama misimbo ya usomaji ya Barthes. Barthes alikuza dhana kwamba, kila hadithi hujumuisha zaidi ya msimbo mmoja. Wingi wa misimbo ndiyo humsisimua msomaji wa matini za kifasihi kusoma kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Kulingana na Barthes, ili kupata maana husishi na maana nasibishi ya ishara, ni sharti mfasiri wa ishara azingatie uhusiano uliopo baina ya ishara na kiashiriwa. Katika *Mythologies* (1957), Barthes anashadidia suala la kuzingatia mazingira na utamaduni wa kijamii ambamo matini zinazochanganuliwa zimeibukia. Kulingana naye, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi zikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara, dhamira na maarifa ya kijamii alionayo mfasiri wa ishara. Mfasiri wa ishara basi anahitaji kutumia hekima pamoja na maarifa ya kijamii kuifasiri ishara inayochanganuliwa kwa kuzingatia elimu ya jamii hiyo. Kulingana na Barthes, kila msimbo ni sauti ambayo imefungamanishwa na matini zinazochunguzwa. Katika, *The Pleasure of the Text* (Barthes 1973), alijadili ya kwamba, hata pale ambapo msomaji wa matini za kifasihi anasoma kwa njia ya kujiburudisha, kuna kiwango ambapo hufika akabaini maana nasibishi ya matini husika katika fikra zake. Aliita hali hiyo ung'amuzi huru. Yaani kuna wakati ambapo mfasiri wa ishara hupata maana ambayo iko kando sana na mazoea yaliyopo. Katika usomaji wa aina hiyo, msomaji wa matini anatafuta vielekezi ambavyo vitamwongoza katika kufikia maana nasibishi ambayo iko nje ya muktadha uliozoeleka. Barthes alijadili kuwa, mielekeo ya kijamii huelekeza namna lugha na mtindo wa uandishi hutumiwa kupitia kazi yake ya, *Writing Degree Zero (*1953). Muundo na mtindo wa mwandishi huathiriwa na mielekeo ya kibinafsi na ile ya kijamii. Baadhi ya ishara zinaweza kufasirika tu kwa kupimwa kwenye mizani ya mielekeo iliyopo. Maana za ishara hubadilika kulingana na mabadiliko ya kiwakati pamoja na matarajio ya wanajamii (Barthes, 1973). Baadhi ya ishara hazihitaji ufafanuzi zaidi ya maana husishi ya ishara.

Katika makala haya, tulitumia misimbo ya ki*seme,* matukio na kiishara.Neno *seme* hutumiwa kuelezea mfumo wa ishara zenye kuleta maana nasibishi katika matini zinazochunguzwa. Msimbo wa ki*seme* pia huitwa msimbo wa kisemantiki. Ishara za kiseme huelezea matukio, wahusika ama mandhari ili kuibua maana nasibishi mbalimbali kwa njia ya uashiriaji. Ishara za kiseme huelezea matukio, wahusika ama mandhari ili kuibua maana nasibishi mbalimbali kwa njia ya uashiriaji kama anavyoshadidia Ali (2013). Msomaji wa matini hung'amua maana nasibishi ya matini kwa kutumia vielekezi mbalimbali vilivyomo katika matini zenyewe. Yaani, matini zenyewe humwelekeza msomaji kwenye maana nasibishi. Maana nasibishi huwa zimetapakaa ndani ya matini yote na hufanya viashirii fulani katika fikra za mfasiri wa ishara na kumfanya kung'amua taswira fulani ya kiashiriwa. Ishara za kiseme hubainishwa na uelewa kwamba, kila ishara huwa na maana husishi na maana nasibishi kutegemea mtumizi, matumizi na muktadha.

Msimbo wa kiishara hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi na nasibishi ya ishara. Ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana nasibishi. Huhusu namna mfasiri wa ishara katika matini za kifasihi huunda wazo (maana) katika fikra zake na jinsi huishia kung'amua maana nasibishi ya ishara. Maana nasibishi inaweza kutokana na majukumu ya ishara husika ama viashiria vyake vingine katika matini. Kila ishara huwa na maana ya kijuuju na maana ya ndani na maana nasibishi hubainishwa na muktadha ama malengo ya matumizi. Msimbo huo pia huitwa msimbo wa vitendo. Kulingana na msimbo wa matukio, tukio moja huwa linaashiria tukio jingine na kujenga maana nasibishi ndani ya matini kwa njia ya kisengerenyuma. Ili kupata maana katika tukio la sasa, ni sharti matukio yote mawili yapatanishwe na kufasiriwa kwa pamoja ili kuibua maana nasibishi inayoashiriwa. Kulingana na msimbo huu, kuna uhusiano baina ya ishara na kinachoashiriwa.

**Mjadala na Matokeo**

Katika kujadili masuala ya kisiasa katika tamthilia ya *Visiki*, makala haya yatajikita katika ufasiri wa ishara mbalimbali na kuibua maana nasibishi ambazo mwandishi anaziashiria kupitia ishara na lugha ya kitamathali kisemiotiki kwa mujibu wa misimbo ya Barthes ya kiseme, kiishara na msimbo wa matukio.

**Siasa za Kikabila na Hila**

Fasihi ni muhimu katika kuelezea hisia za kisiasa kwani huwa ni kipaaza sauti kwa wanyonge katika jamii (Markey, C 1999, Bolongaro, E 2003). Kwa muda mrefu, viongozi wa Kiafrika wamekuwa wakifanya siasa za kikabila na utengano badala ya kuwa wazalendo na siasa za kitaifa. Kwa ajili hiyo, demokrasia haipo. (*Viski* uk 1-7). Hiyo ndio maana ya kisemiotiki kulingana na msimbo wa Barthes wa matukio wakati halaiki inafika kwa mhusika Mungu katika *Visiki.* Suala la umaskini na siasa chafu linabainika kama tatizo kuu katika siasa kwenye nchi za Kiafrika.

NDOVU: Hata hivyo, kukosa chakula siyo hoja. Tutazungumza tu na kucheka pamoja. (*Anajichekesha. Ni wazi kwamba Huzuni haelewi*) Sisi ni watu wa kabila moja…Lazima ujali.Karibu tutaangamizwa.Kabila letu litaangamizwa na Wavirindwa.

Kulingana na Barthes, kila msimbo ni sauti ambayo imefungamanishwa na matini zinazochunguzwa. Katika, *The Pleasure of the Text* (Barthes 1973), alijadili ya kwamba, hata pale ambapo msomaji wa matini za kifasihi anasoma kwa njia ya kujiburudisha, kuna kiwango ambapo hufika akabaini maana nasibishi ya matini husika katika fikra zake. Aliita hali hiyo ung'amuzi huru. Yaani kuna wakati ambapo mfasiri wa ishara hupata maana ambayo iko kando sana na mazoea yaliyopo'… Kabila letu litaangamizwa na Wavirindwa' kulingana na misimbo ya matukio na msimbo wa kiishara ina maana nasibishi kuwa, wanasiasa ndio huchochea uhasama miongoni mwa wananchi na kuanzisha vita vya kimbari katika mataifa ya Kiafrika. Chanzo cha uongozi hafifu basi ni hila za viongozi na kukosa elimu ya kisiasa miongoni mwa umma katika nchi hizi. Wanasiasa hawajali kutamaukiwa kwa wananchi wao. Kukosa tumaini, kukosa chakula na mavazi ni suala la kawaida katika mataifa mengi.

MUNGU: ..Nanyi mngetumia akili zenu kukataa.(*kimya*). Nilipomwumba binanadamu, nilimpa kila mmoja macho ya kuona, Masikio ya kusikia, Mdomo wa kukana na kukubali, Ubongo wa kufikiri

Kulingana na Barthes, ili kupata maana husishi na maana nasibishi ya ishara, ni sharti mfasiri wa ishara azingatie uhusiano uliopo baina ya ishara na kiashiriwa. Katika *Mythologies* (1957), Barthes anashadidia suala la kuzingatia mazingira na utamaduni wa kijamii ambamo matini zinazochanganuliwa zimeibukia. Kulingana naye, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi zikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara, dhamira na maarifa ya kijamii alionayo mfasiri wa ishara.Ishara ya 'kimya' na mhusika Mungu kisemiotiki inaashiria onyo kwa umma katika nchi za Kiafrika. Wananchi wanastahili kujichunga na hila za wanasiasa na kuwajibikia majukumu ya kisiasa ambayo wanayatekeleza. La sivyo, ni wao ndio watajilaumu iwapo kutakuwa na machafuko ya kisiasa ama kunapotokea uongozi duni nchini mwao.

Kikwazo kikuu kwa siasa endelevu katika mataifa mengi ya Kiafrika basi ni ukabila. Viongozi wengi hawana sera za kitaifa. Wanasia ndio waporaji wakubwa wa mali za taifa.

NDOVU: Tatizo lako kubwa ni kule kusahau kabila lako…Kabila letu litaangamizwa na Wavirindwa (*Visiki* uk wa 41)

'… kusahau kabila lako' ni ishara ya kiashiria kulingana na msimbo wa Barthes. Kazi ya fasihi huwa na majukumu ya kuizindua jamii na kuipa (Senkoro 1988, Wamitila 2003 na Iribemwangi na Mukhwana 2011). Huu ndio wajibu unaotekelezwa na mtunzi wa *Visiki.*

**Chaguzi Ghushi na Udanganyifu**

Kama wanavyopendekeza Markey (1999) na Eugenio (2003), haiwezekani kubadilisha namna siasa zinafanywa bila kusahihisha tatizo la muda mrefu la chaguzi ambazo ni za kuhadaa umma na kuwafaidi matapeli wa kisiasa pekee kama inavyoashiriwa katika *Visiki.* Wakati umefilka ambapo viongozi wanaochaguliwa kukoma kujiona kama miungu bali watumishi wa umma.

HUZUNI: Lakini hatukutarajia kuwa Ndovu atazisaliti nafsi zetu.

MATANGA: Nasi tuliwabeba wanasiasa hao kwa migongo yetu (*Kimya*)…Wanapohitaji kura wao hutuahidi mashamba makubwa. Lakini wapi?

Kulingana na Barthes, ili kupata maana husishi na maana nasibishi ya ishara, ni sharti mfasiri wa ishara azingatie uhusiano uliopo baina ya ishara na kiashiriwa. Katika *Mythologies* (1957), Barthes anashadidia suala la kuzingatia mazingira na utamaduni wa kijamii ambamo matini zinazochanganuliwa zimeibukia. Kulingana naye, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi zikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara, dhamira na maarifa ya kijamii alionayo mfasiri wa ishara. 'Kimya' baada ya maneno ya Matanga ni ishara ya kisemiotiki yenye kuashiria tafakuri za majuto ya mpiga kura katika nchi za Kiafrika. Umuhimu wa wananchi wapiga kura huisha baada ya kupiga kura. Hila za viongozi wa kisiasa hubainika mara tu baada ya kuingia bungeni: wananyakua mashamba, wanawapiganisha wapiga kura kikabila na kitabaka na hawajali umoja wa kitaifa. 'Nasi tuliwabeba wanasiasa hao kwa migongo yetu' ni ishara ya kimatukio kulingana na Barthes. Kulingana na msimbo wa matukio, tukio moja huwa linaashiria tukio jingine na kujenga maana nasibishi ndani ya matini kwa njia ya kisengerenyuma. Wakati viongozi wanatafuta kura, hujifanya kuwa wanawajali wananchi na kuahidi kuwaletea ustawi na maendeleo makubwa. Hata hivyo, kutokana na hila za viongozi, hali hiyo husalia kuwa ndoto tu. Maana nasibishi ni kuwa, viongozi wa kisiasa katika nchi nyingi za Kiafrika, hawatimizi ahadi wanazozitoa kwa umma. Umma basi huwa umesalitiwa. Asasi ya bunge katika mataifa haya huwa ni mahali pa wanasiasa kupitishia ajenda zao na sio za umma mara nyingi. Ikifasiriwa kwa msimbo ya Barthes inaibuka ya kwamba, siasa za ahadi nyingi katika nchi za Kiafrika lazima zikome. Lazima kuwe na usawa katika utumizi wa maliasili ya nchi.Hiyo ndiyo maana nasibishi kisemiotiki kwa mujibu wa msimbo wa kisemantiki.

**Siasa za Kuteka Umma Nyara na Utabaka wa Kisiasa**

Njaa na utepetevu wa chakula kwa muda mrefu vimetumiwa kama silaha ya kisiasa wakati wanasiasa wanatafuta umaarufu wa kisiasa katika nchi nyingi za Kiafrika. Tabaka la kisiasa limekuwa likishikilia mamamlaka kwa kila njia bila kujaji matatizo ya umma kama ukosefu wa vyakula na mavazi. Miradi ya maendeleo kama upanzi wa maua vimekuwa ukiwafaidi wanasiasa pekee ijapo ni wananchi ndio wamekuwa wakitoa jasho lao ili kuzalisha mali husika.

MATANGA: Maua ni chakula cha nyuki. Nyuki wakila maua hutengeneza asali. (*Kwa hasira*). Lakini hata sisi tunataka kibuyu kidogo cha asli hiyo.(*Visiki* uk wa 18)

'Hasira' ikifasiriwa kwa mujibu wa msimbo wa Barthes wa ki-ishara inaibua maana nasibishi kuhusu unafiki wa kisiasa na hila za wanasiasa kuhusu umma wao. Kulingana na msimbo huu, maana nasibishi inaweza kutokana na majukumu ya ishara husika ama viashiria vyake vingine katika matini kulingana na msimbo huu. 'Hasira' ya wananchi inatokana na kwamba, raslimali za kitaifa zinawafaidi wanasiasa wachache na sio mwananchi wa kawaida. Pesa zinazotokana na mapata ya kigeni zinafaidi tabaka la viongozi pekee huku umma ukiangamizwa na umaskini. Siasa za nchi nyingi za Kiafrika zinaendeleza ukandamizi wa umma na raslimali hazigawanywi kwa usawa. Hii ndio sababu siasa za nchi nyingi barani bado ni duni na hakuna usawa wa kitaifa.

Kulingana na Markey (1999) na Eugenio (2003), uongozi duni unatokana na mifumo mibaya ya kiuchumi na kukosekana na sera za kitaifa kuhusu uongozi. Kulingana na msimbo wa matukio, fasiri ya tukio hili inachipua maana nasibishi kuwa, mwananchi katika mataifa ya Kiafrika ametamaukiwa kisiasa na sasa amepoteza tumaini. Ithibati iliopo ni kuwa, pale ambapo hapana usawa wa kisiasa na ustawi, vita vya kimbari vinaweza kutokea na kusababisha vifo vya halaiki kama ilivyotokea nchini Rwanda mnamo 1994. Wanasiasa wahuni hutumia umaskini wa watu kuwatenga kikabila na kuanzisha vita vya kikabila (*Visiki* pg 47-50).

**Maadili ya Kisiasa Yaliyopitwa na Wakati**

Kutawaliwa na mkoloni hakuwezi kuwa kisingizio cha mara kwa mara cha uongozi duni katika mataifa ya Kiafrika. Ni lazima Waafrika wabuni njia mbadala na masuluhisho ya kiteknolojia kulingana na matakwa yao. Kukariri ukoloni kama sababu ya kufifia kisiasa na kijamii basi ni suala lililopitwa na wakati Afrika.

MWALIMU: Ni kwa sababu walituvamia na kututawala.Walitudhulumu na kuchelewesha maendeleo yetu. (*Visiki* uk wa 23)

Ikifasiriwa kwa kutumia msimbo wa matukio, kuna maana nasibishi kuhusu unafiki wa kisiasa na propaganda ambazo viongozi wanatumia kufidia udhaifu wao kisiasa. Huu ni ulaghai wa kisiasa kwa umma (*Visiki* uk 29). Mawazo ya mhusika Mwalimu yanayokaririwa na mwanafunzi wake Majaliwa, yakifasiriwa kisemiotiki yanaashiria ushinde na kukosa tumaini kwa wananchi wengi katika mataifa ya Kiafrika. Viongozi hawazingatii uhalisia ulivyo.

MAJALIWA: Ilikuwa katika somo la historia…Mwalimu alitufundisha kuwa, watu wa kwanza kuishi duniani walikuwa watu weusi. Waliishi katika konde kubwa la Mto Nile hapo zama za kale...ni sisi tuliovubua maarifa mengi yajulikanayo duniani sasa. Ni sisi tuliovumbua maarifa ya kuandika…(*Visiki* u.k 23)

Ishara za kiseme huelezea matukio, wahusika ama mandhari ili kuibua maana nasibishi mbalimbali kwa njia ya uashiriaji kama anavyoshadidia Ali (2013). Lazima Waafrika wafanye uvumbuzi wa kiteknolojia inayoafiki matakwa na mahitaji yao wenyewe badala ya kutegemea mataifa ya kimagharibi na kuzidi kulalamika. Elimu ya kukariri pekee mawazo haiwezi kusuluhisha matatizo ya bara hili kisiasa bila kuonyesha ukakamavu wa kisiasa na viongozi na kubuni sera za kitaifa ambazo ni tekelezi. Kulingana na msimbo wa kiishara wa Barthes, maana nasibishi inaweza kutokana na majukumu ya ishara husika ama viashiria vyake vingine katika matini. Kila ishara huwa na maana ya kijuuju na maana ya ndani na maana nasibishi hubainishwa na muktadha ama malengo ya matumizi. Majaliwa anaashiria ukengeushi ambao umma katika mataifa ya Kiafrika yameathirika kwao. Badala ya wanafunzi baada ya shule kuwa watekelezaji, na wavumbuzi, ni kasuku wanaokariri mawazo tu. Aidha kuna haja ya kuwa na mifumo faafu ya elimu yenye kusudi la kukwamua maendeleo.

Afrika inahitaji siasa za muunganiko, kuimarisha miundomisingi na kuondoa njaa na ukabila.

BI. TAMAA: (*Ni dhahiri kuwa anasema uongo*) chanzo cha matatizo yenu ni Makaburu…sisi (viongozi) twajitahidi tuwezavyo lakini makaburu hawatatuacha (*Visiki* uk 29)

Kulingana na msimbo wa matukio, tukio moja huwa linaashiria tukio jingine na kujenga maana nasibishi ndani ya matini kwa njia ya kisengerenyuma. Kwa muda mrefu, viongozi wa Kiafrika wanaposhindwa na uongozi, huyasingizia mataifa ya kigeni hasa koloni za kitambo. Huenda ni kutokana na kwamba, kupitia mifumo ya elimu ambayo mingi bado inatumika barani ni ile iliyoanzishwa na hao wakoloni. Hii ndio inaashiriwa na 'chanzo cha matatizo yenu ni makaburu…' Ni dhahiri kwamba, huu ni uongo wa viongozi wasio na maadili ya kitaifa. Mhusika Mwalimu akifasiriwa kwa kutumia msimbo wa kiishara basi, anaashiria suluhisho ambalo mataifa ya Kiafrika yanahitaji ili kubadilika kisiasa. Lazima mataifa ya Kiafrika yaanzishe mifumo ya elimu ambayo inahimiza kupata maarifa na kusuluhisha matatizo na sio kukariri maarifa tu. Mnamo mwaka wa 2017, Kenya ilianzisha mfumo wa elimu ya kiamilifu (CBC) kama njia ya kujaribu kubadilisha hali husika.

**Suluhu kwa Siasa Duni na Uongozi**

Mkutadha ambamo ishara inayofasiriwa huchipukia huwa na athari kwa ujumbe unaowasilishwa na namna ujumbe huo huishia kufasiriwa na mhakiki. Mabadiliko ya kiwakati huwa na uwezo wa kuathiri matini za kifasihi kidhamira, kimaudhui na kifani (Shariff 1988). Taifa linapokuwa maskini, viongoi hupata mwanya wa kuugawanya umma, uchochezi na propaganda, kukuza ukabila, unyakuzi wa ardhi na kutumia vyombo vya dola kumnyanyasa mwananchi wa kawaida na uskwota. Suluhu ya kudumu ni kuondoa umaskini, ukabila, utabaka na matumizi mabaya ya mamlaka.

NAUTUTU: Mwanangu alikufa hali sisi tumetazama…nasi tulifahamu ni njaa, hali tusiwe na la kufanya

HUZUNI: Na siyo kwamba ardhi haipo. La, ardhi ipo (*Visiki* uk.9-10)

Kulingana na misimbo ya Barthes, ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana nasibishi. Huhusu namna mfasiri wa ishara katika matini za kifasihi huunda wazo (maana) katika fikra zake na jinsi huishia kung'amua maana nasibishi ya ishara. Watoto kufa njaa na kuna ardhi kunaashiria kisemiotiki dhuluma na kukosekana kwa uwajibikaji kutoka kwa

viongozi katika nchi nyingi za Kiafrika. Mbali na tatizo la raslimali, kuna ufisadi na unyanyasaji kutokana na matumizi mabaya ya vyombo vya dola.

ASKARI 2: Haja yetu ni kuhakikisha tuna kazi kila siku.Hivyo tukipata skwota… aliyetayari kujitengenezea jina,btunapokea…(*Visiki* uk. 17)

Kulingana na Barthes, maana nasibishi huwa zimetapakaa ndani ya matini yote na hufanya viashirii fulani katika fikra za mfasiri wa ishara na kumfanya kung'amua taswira fulani ya kiashiriwa (Barthes 1970). Ishara za kiseme hubainishwa na uelewa kwamba, kila ishara huwa na maana husishi na maana nasibishi kutegemea mtumizi, matumizi na muktadha. '...aliyetayari kujitengenezea jina, tunapokea..' ni ishara ya kiseme. Vyombo vya dola vinakula hongo badala ya kutekeleza haki kwa umma kwa sababu vimetekwa nyara na wanasiasa.

**Hitimisho**

Kupitia makala haya, tulibaini kwamba siasa katika mataifa ya Kiafrika ni duni na chaguzi zimejaa udanganyifu. Ukabila na umaskini ni silaha ya wanasiasa kuwapiganisha wapiga kura. Hakuna usawa katika ugawanyaji wa raslimali za kitaifa na watu wengi wanaangamia katika vita vya ikabila na majanga ya njaa na kukosa mahitaji ya kimsingi kama nguo. Badala ya viongozi kutafuta suluhlu za kisiasa, wanayatumia mataifa ya kimagharibi kama kisingizio kwa njia za kipropaganda. Kuna kukariri mapisi na maarifa badala ya utekelezaji.

**Marejeleo**


Akaranga, S. D. I. (1987). *Semi za Kiswahili: Maana na Matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.

Ali, M. (2013). *Jadeed adbi tanqidi nazarya*. (Sindhi). Sukhar: My Publication Press.

Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi: Oxford University Press.

Arege, T., & Matei, A. (2005). *Kunga za Kiswahili 3: Kitabu cha Mwanafunzi*. Nairobi: FocusPublishers.

Atkin, A. (2013). *Peirce's Theory on Signs*. Stanford Encylopedia of Philosophy.

Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory.* Manchester: Manchester University Press.

Barthes, R (1957). *Mythologies*. New York: Hill & Wang.

Barthes, R (1967). *Elements of Semiology* (trans. Annette Lavers & Colin Smith). Jonathan Cape.

Barthes, R. (1964). *Elements of Semiology*. New York: Hill and Wang.

Barthes, R. (1968). *Elements of Semiology* (1st Ed.). New York: Hill and Wang.

Barthes, R. (1974). S/Z. (R. Miller, Trans.) United Kingdom. Blackwell Publishing Ltd.

Barthes, R. (1981). "Theory of the Text" Ian Macleod (Trans. Katika R. Young (Ed.), *Untying the Text*. London: Routledge.

Barthes, R. (1997). Image-Music-Text. S. Heath (Ed.). *The Journal of Aesthetics and Criticism* (Vol. 37), (220.) Hill and Wang.

Barthes, R. (2016). https://monoskop.org/images/2/2c/Barthes_Roland_Elements_of_Semiology_1977.pdf

Bradford, R. (1977). Stylistics. *The Critical Idiom.* London: Routledge.

Charles, S. H. (1977). *Semiotic and Significs*: *The Correspondence between Charles S. Peirce and Victoria Lady Welby*. Indiana: Indiana University Press.

Chiraghdin, S. & Mnyampala, M. (1977). *Hisitoria ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Chiraghdin, S. (1974). Kiswahili na Wenyewe. *Mulika, 6*, 35-41. Nairobi: Oxford University.

Jakobson, R. (1985). *Selected Writings*. Stephen Rudy (Ed.). Paris: Mouton.

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Khaemba, O. (1984). *Visiki*. Nairobi: EAE Publishers.

Kingei, G. K. & Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Lambert, H. E. (1957). *Ki-Vumba, a Dialect of the Southern Kenya Coast.* Kampala: East African Swahili Committee, Makerere College.

Lambert, H. E. (1965). Some Intiation Songs of the Southern Coast. Swahili, *35*(1), 49-67.

Maliki, A. (2019). Alustath Journal for Human &Social Science. Vol. 58, issue 3. (uk. 403-434)

Mckay, W. F. (1975). *Pre-Colonial History of the Southern Kenyan Coast.* Unpublished PhD, Dissertation, Boston University.

Mohamed S. M. (1978). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press.

Ndalu & King'ei, G. (1989). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: EAEP.

Ryan, A. (2012). *On Politics: A History of Political Thought from Herodotus to the Present.* London: Allen Lane.

Sanja, L. W. L (2022). *Uhakiki wa Ishara na Tamathali Katika Ushairi, Masimulizi na Semi: Mtazamo wa Kisemiotiki wa Fasihi ya Kivumba*. Unpublished Thesis, Kenyatta University.

Sanja, L. W. L. (2020). Taasubi Katika Shirikina za Kivumba: Mtazamo wa Kisemiotiki. *Jarida la Mwanga wa Lugha, 5*(2), 165-74.

Sanja, L. W. L., & Others (2022). Siasa, Uchumi na Ustawi wa Jamii: Mtazamo wa Kisemiotiki wa Ushairi wa Kivumba. *Jarida la Mwanga wa Lugha*, *7*(1), 89-103.

Sanja, L. W. L., Kitula, K., & Wafula, R. (2020). Socio-Economic, Political and Religious Realties: Semiotic Interpretation of Selected Kivumba Oral Narratives. *International Journal of Creative Research and Studies (ITJCRS), 4*. ISSN-0249-4655.

Sanja, L. W. L., Kitula, K., na Wafula, R. (2020). Semiotic Survey of Kivumba Superstitions. *International Journal of Innovative Research and Knowledge, 5*(5). ISSN- 2213-1356.

Senkoro, F. M. K. (1984). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. M. K. (2012). *Fasihi kwa Watoto wa Kitanzania*. Mswada. Haujachapishwa.

TUKI (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Van der Eijk, C. (2018). What is Politics? *The Essence of Politics*. Amsterdam: Amsterdam University Press, 9–24.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (2011). *A Dictionary of Stylistics* (3rd Ed.). London: Routledge.

Wamitila, K .W. (2002a). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipera Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K .W. (2002b). *Kamusi ya Misemo na Nahau*: *Lulu za Lugha 1*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K .W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.